JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Mtaa wa Kingóla
S.L.P 845,
67109 MOROGORO
Simu: 023-2614302
Nukushi: 023-2614478
Simu ya Bure: 113 au *113#
Barua pepe: rbcmorogoro@pccb.go.tz
Wavuti: www.pccb.go.tz

TAARIFA KWA UMMA KUPITIA VYOMBO VYA HABARI

MOROGORO Oktoba 09, 2020

TAKUKURU MORO YARUDISHA TABASAMU KWA WANYONGE

Ndugu Waandishi wa Habari,

Kipindi cha miezi mitatu tangu kuwahabarisha Wananchi wa Mkoa wa Morogoro kupitia vyombo vya habari juu ya utendaji kazi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoa wa Morogoro kimepita. Leo tunatoa taarifa ya utendaji kazi kwa kipindi cha kuanzia mwezi **Julai 2020 hadi Septemba 2020.**

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyeturuzuku zawadi ya uhai na afya njema inayotuwezesha kuendelea kuwatumikia wenzetu kwa moyo wote.

Pili, niwashukuru sana wanahabari wote kwa kuitikia wito wetu na kuja kupata habari ambazo mtazifikisha kwa wananchi ambao wataendelea kufahamu namna Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoa wa Morogoro inavyotekeleza majukumu yake. Kitendo hiki

kinathibitisha ushiriki wenu wa moja kwa moja katika mapambano dhidi ya rushwa katika Mkoa wetu wa Morogoro.

Ndugu wandishi wa Habari

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Morogoro kwa kuzingatia majukumu mtambuka iliyopewa kisheria imeendelea kuongeza nguvu kupigania haki za wananchi wanyonge waliokuwa na kadhia mbalimbali ikiwemo kudhulumiwa haki zao kwa namna tofauti.

Kwanza, TAKUKURU Morogoro imefanikiwa kurejesha matofali zaidi ya **Elfu Kumi na Mbili na Mia Nne (12,400)** kwa wanakijiji wa Pulambili katika Kata ya Kidugalo Mkoani Morogoro. Awali ilikubaliwa na wanakijiji hao kuwa kijiji kipime na kuuza viwanja 53 ambapo baada ya mauzo hayo fedha kiasi cha Shilingi Milioni Moja Mia Nane na Hamsini na Tano Elfu **(Tshs. 1,855,000/=)** zilipatikna; kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi **Laki Sita na Kumi na Tano Elfu (Tshs. 615,000/=)** tu ziliwasilishwa ofisini na Mwenyekiti wa kijiji ambaye ndiye alikuwa na dhamna ya kuzipokea. Kiasi kingine za shilingi **Milioni Moja Mia Mbili na Arobaini Elfu (Tshs. 1,240,000/=)** hakijulikani kilipo. TAKUKURU ilipochunguza ilibaini kuwa mwenyekiti huyo kahusika hivyo ilimtaka afyatue matofali yenye thamani ya fedha hiyo naye alifanya hivyo. Mnamo tarehe 17/09/2020 chini ya usimamizi wa TAKUKURU matofali 12,400 yalikabidhiwa kwa wananchi wa kijiji cha Pulambili.

Kwa kitendo hicho ni dhahiri kuwa mwenyekiti aliyekuwa na dhamana alivunja uaminifu na kufanya matumizi binafsi ya fedha hizo kinyume

na matarajio na lengo zuri la wananchi waliokusudia kuisaidia Serikali yao ili kujiletea maendeleo yao.

TAKUKURU inatoa onyo kwa viongozi wote wa aina hii katika Mkoa wa Morogoro na kuwataka kuacha tabia hiyo.

Pili, TAKUKURU imeweza kurejesha fedha kiasi cha Shilingi **Milioni Ishirini (Tsh 20,000,000/=)** kwa wakulima wa Miwa ambao ni wanachama wa Mtibwa Outgrowers Association (MOA) na TUCOCPRCOS LTD wa Turian, Wilayani Mvomero. Wakulima hao walikuwa wanavidai vyama hivyo fedha zaidi ya **Shilingi Milioni Mia Moja na Moja Mia Tisa Themanini na Tisa Elfu Mia Nne Tisini na Nne na Senti Arobaini na Sita** [**Tsh 101,989,494.46]** wanachama wa MOA na **Shilingi Milioni Mia Moja na Kumi na Sita Mia Sita Kumi na Nane Elfu Mia Mbili Arobaini na Saba** [**Tsh 116,618,247.00]** wanachama cha TUCOCPRCOS LTD fedha hizo ni mauzo ya miwa yao kupitia vyama vyao kwenda kiwanda cha Sukari Mtibwa (**Mtibwa Sugar Estates - MSE**). Malalamiko yao yalifika TAKUKURU ndipo, tulifanya ufuatiliaji na kubaini uwepo wa tatizo hilo. Kwa sasa jumla ya fedha kiasi cha Shilingi **Milioni Arobaini na Tatu Laki Nane (Tsh 43,800,000/=)** zimerejeshwa na kiasi kilichobaki TAKUKURU itahakikisha kinarejeshwa chote.

Tatu, katika kudhibiti uonevu wa vikundi vinavyojihusisha na ukopeshaji wa fedha pasipokufuata utaratibu, tumeweza kumrejeshea nyumba yake mwananchi wa kijiji cha Ihenje kilichopo Wilayani Gairo ambayo alipokonywa na mfanyabishara baada ya kushindwa kumlipa

deni la shilingi **Laki Moja na Elfu Hamsini (150,000/=)** ambazo alimkopesha.

Mkataba huo ulikuwa ni wa makubaliano ya miezi sita ambapo ingetimia mkopaji huyo alipaswa kulipa shilingi laki tatu. Dhamana ya mkopo huo ilikuwa ni nyumba ya vyumba viwili iliyojengwa kwenye eneo la ukubwa wa takribani zaidi ya robo eka. Hata hivyo kabla ya kipindi cha mkataba kwisha mfanyabiashara huyo akamtaka mkopaji arejeshe fedha yake yote.

Baada ya mahangaiko mengi katika vyombo vya usuluhishi mkopaji aliamuriwa kumkabidhi mfanyabishara huyo dhamana ambayo ni nyumba na eneo lilipojengwa. Mfanyabiashara huyo alimpa kipindi cha maandalizi ya kutoka katika nyumba ya mkopaji kwa kumpangisha kwenye ile nyumba yake kwa kodi ya shilingi **Elfu kumi (Tsh 10,000/=)** kwa kila mwezi.

TAKUKURU ilishughulikia na imefanikiwa kumejeshea nyumba mnyonge huyo ambapo yeye atawajibika tu kulipa thamani halisi ya deni na riba ya asilimia ishirini tu tofauti na mkataba wa awali. Utekelezaji huo utafanyika ifikakapo 30/10/2020 na utazingatia kipindi cha Desemba 2017 hadi Juni 2018

TAKUKURU pia imerejeha shamba lenye ukubwa la ekari moja na nusu lililopo Wilayani Gairo ambalo lilikuwa ni la urithi ambapo liliuzwa na mtoto wa kiume wa marehemu kinyume na utaratibu.

Nne, Tukio lingine la dhuluma linamuhusu bibi mjane aitwaye **NG'WALU KUDEBHA** mwenye umri wa miaka sabini (70) ambaye alidhulumiwa shamba lake lenye ukubwa wa ekari 15. Shamba hilo lilinuliwa na mjane huyo mwaka 2019 kutokana na fedha yake kiasi cha **Shilingi Milioni Nne (Tsh. 4,000,000/=)** alizozipata baada ya kuuza ngómbe wake pamoja na eneo alilokuwa akiishi katika kijiji cha Kalanga Kata ya Malya Wilaya ya Kwimba Mkoani Mwanza kufuatia uamuzi wake wa kuhamia Wilaya ya Malinyi Mkoani Morogoro kwa shughuli za kilimo baada ya mume wake aliyekuwa akimtegemea kufariki dunia.

Ununuzi huo ulihusisha mkwe wa bibi mjane huyo ambapo baada ya bibi huyo kuhamia na kukaa katika eneo hilo, mkwe huyo alimgeuzia kibao Bi NG'WALU KUDEBHA na kumtaka ahame kwenye eneo lake hilo kwa madai kuwa shamba hilo si mali yake na hakulinunua yeye. Msingi wa madai hayo ulibainishwa na uchunguzi wa TAKUKURU kuwa ni kitendo cha mkwe wa Bi NG'WALU KUDEBHA kuandika jina la mke wake yaani mtoto wa bibi huyo na kusema eneo hilo ni lao. Bi NG'WALU KUDEBHA alipeleka malalamiko yake katika vyombo mbalimbali ya usuluhishi bila mafanikio mpaka TAKUKURU ilipoingilia kati ambapo katika uchunguzi wake ilibainika kuwa Bi NG'WALU KUDEBHA ni kweli alituma fedha zake za ununuzi wa shamba akishuhudiwa na mashahidi na kuthibitishwa na ushahidi wa kumbukumbu za michakato ya utumaji wa fedha hizo mamlaka husika.

Mnamo tarehe **18/09/2020** TAKUKURU imemkabidhi shamba lake Bi **NG'WALU KUDEBHA** baada ya mkwe wake huyo kukiri kuwa ni kweli alimdhulumu.

TAKUKURU Morogoro inatoa wito kwa wanajamii wote kuheshimu haki za wajane na makundi mengine maalumu hususani katika umiliki wa rasilimali ardhi ambao ndio tegemeo la maisha ya wanyonge. Tatizo hili linaonekana kushamiri sana katika baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Morogoro. **TAKUKURU** inawataka viongozi wa mamlaka ya Serikali za Mitaa katika ngazi za chini kusimamia kikamilifu ulinzi wa haki za wajane na wote wanaodhulumiwa katika mazingira kama haya.

TAKUKURU haitasita kuchukua hatua kali sana dhidi ya watu wanaojihusisha na vitendo hivyo ambavyo vinachagizwa na rushwa kwa lengo la kuhakikisha kuwa wafanya dhuluma wanaziba midomo baadhi ya watendaji wasio waadilifu wa vyombo vya haki hususani ngazi za chini za mabaraza ya ardhi na usulihishi.

UELIMISHAJI UMMA

Ndugu Waandishi wa Habari,

Katika uelimishaji Umma TAKUKURU imekuwa ikitoa mafunzo ya rushwa, maadili na wajibu wa wananchi katika mapambano dhidi ya rushwa kwa lengo la kuwahamasisha wananchi wote ili waweze kushiriki katika kudhibiti vitendo hivyo. Katika kipindi hicho mkazo ulitolewa kwa wanachama wa vyama vya siasa hususani wanalioshiriki katika upigaji wa kura za maoni pamoja na wagombea wa nafasi za teuzi mbalimbali kwa lengo la kushiriki katika kinyangányiro cha uchaguzi Mkuu 2020 unaohusisha madiwani, wabunge na Rais ili kujiepusha

kushiriki vitendo vya rushwa vyenye mrengo wa kuchagua viongozi wasio na sifa na wasiolenga kutetea maslahi ya taifa kwa kuleta maendeleo kwa wananchi. Elimu hiyo ilitolewa kwa njia ya mikutano ya hadhara, semina uandaaji na urushaji wa vipindi vya redio na Television.

Ndugu Waandishi wa Habari,

Katika kipindi cha Mwezi **Julai 2020 hadi Septemba 2020**, tumeendelea kupokea malalamiko mbalimbali toka kwa wananchi na malalamiko yanayohusu vitendo vya rushwa, chunguzi wake bado unaendelea na pindi ushahidi utakapopatikana wahusika watachukuliwa hatua kali za kisheria na kinidhamu. Aidha yasiyohusiana na rushwa, TAKUKURU imeyashughulikia kwa kuhusisha taasisi husika zenye wajibu wa kuwashughulikia wananchi hao na kutatua kero zao.

TAKUKURU inatoa wito kwa watendaji wote wa umma Mkoani Morogoro kutimiza wajibu wao kikamilifu ili kuwapunguzia kero wananchi ambao wana dhamana ya kuwatumikia.

MIKAKATI YA VIPAUMBELE KWA KIPINDI CHA KUANZIA MWEZI OKTOBA 2020 – DESEMBA 2020

Ndugu Waandishi wa Habari

kwa kipindi cha **Oktoba 2020 hadi Desemba 2020** tumejiwekea mikakati kadha wa kadha ikiwemo kuendelea kutoa elimu ya vitendo vya rushwa kwa wananchi ili watumie haki yao kidemokrasia ya kuchagua viongozi waadilifu na wasiojihusisha na vitendo vya rushwa watakao simamia na kuletea maendeleo kwa wananchi wao.

TAKUKURU inatoa wito kwa wananchi kushiriki katika mikutano ya kampeni inayoendelea kwa sasa ili waweze kusikiliza sera za wagombea na kufanya maamuzi stahiki ifikapo siku ya uchaguzi tarehe 28 Mwezi Oktoba Mwaka 2020. Siku hiyo pia wajitokeze kwa wingi kupiga kura kwa manufaa ya taifa lao. TAKUKURU inaendelea kuwakumbusha wananchi wote kuacha kurubuniwa ili wauze shahada zao za kupigia kura. Hilo sio tu linawezapoteza haki yao ya msingi ya kuchagua viongozi wanaowataka bali pia linaathiri demokrasia.

TAKUKURU pia itaendelea na kazi ya kufuatilia kampuni zinazokwepa kulipa kodi ikiwemo kampuni ya ujenzi iliyokwepa kulipa kodi ya ongezeko la Thamani ***(VAT)*** baada ya kuingia mkataba na TARURA ili iweze kujenga barabara za Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro.

Kwa ujumla wake TAKUKURU itaendelea kuwapigania wahanga wote wa Rushwa hususani wanyonge wanaodhulumiwa.

Ni rai yetu kuwa wajitokeze kwa wingi kutoa taarifa TAKUKURU kupitia namba ya simu ***113#, 113** au **0738 150 143 au kufika katika Ofisi za TAKUKURU Morogoro zilizoko Mtaa wa Kingóla na ofisi zilizopo kila wilaya**

Ninawashukuru sana kwa kunisikiliza.

Imetolewa na:

Janeth Machulya

MKUU WA TAKUKURU (M),
MOROGORO